

»Mpango wa Biashara wa Kilimo cha Koliflawa— Jinsi ya Kukuza Koliflawa— Biashara ya Kilimo cha Mboga«

Koliflawa ni mboga yenye lishe ya vitamini. Wingi na ubora wake umedhamiriwa na aina na kiwango cha teknolojia inayotumiwa.

Kilimo cha koliflawa ni biashara yenye thamani ya juu ya lishe na manufaa ya kiafya, mahitaji yake ni makubwa na kwa upangaji sahihi na utunzaji ufaao, upanzi una ghamama ndogo. Pia inahitaji kazi kidogo na ni biashara yenye faida zaidi.

Usimamizi wa mazao

Zao la koliflawa hukua vizuri katika aina zote za udongo hasa mchanga ,udongo tifutifu na udondo mfinyanzi. Miche huinuliwa kwenye vitalu na kupandwa kwenye shamba lenye ukubwa wa mita 1 upana na wa mita 3 kwa urefu ambalo hutayarishwa kwa kuchanganya mchanga, udongo na samadi. Changanya mbolea ya muriate na mbolea ya TSP vizuri siku 8 kabla ya kupanda na baadaye weka yurea kwa ukuaji mzuri wa miche.

Wakati wa kuandaa ardhi inapaswa kulima kwa kina mara 4–5, nyunyiza mbolea inayohitajika kwenye ardhi na kuchanganya na udongo. Kwa ardhi iliyotayari, kitanda kinapaswa kuwa senti mita 15–20 kutoka ardhini na upana wa mita 1. Miche ya majani 5–6 hupandwa kwenye shamba kuu baada ya siku 30–35 za kupanda kwa umbali wa sm 60*45 hasa mchana na kisha weka mbolea.

Kuweka mbolea

Mbolea huwekwa kwa awamu 3 ambazo ni siku 10 baada ya kupanda, siku 25 na wakati wa kuunda kichwa cha mmea. Mwagilia ardhi

maji baada ya kuweka mbolea na baada ya siku 2–3 vizuri kisha weka dawa za kuulia wadudu na magugu kabla ya kupandikiza ikifuatiwa na kupalili kwa mkono na siku 42 baada ya kupandikiza.

Hatimaye, unganisha majani pamoja juu ya kichwa ikiwa na upenyo wa takriban inchi 2–3 ili kusawazisha na kulinda mmea kutokana na joto na kudumisha rangi nyeupe ya matunda .Weka dawa za kuuwa kuvu na za kuuwa waduduna magugu ili kudhibiti wadudu na magonjwa na kuvuna wakati matunda yamekomaa hasa wakati wa asubuhi na mchana.